


Mwongozo wa Maelekezo ya iPad



Swahili

Muhtasari wa iPad

iPad yako huletwa kutoka Apple ikiwa na karatasi ya maelekezo katika kisanduku.


Mwongozo kamili wa Mtumiaji wa Apple unapatikana mtandaoni kwenye support.apple.com Mwongozo huu ambao unasoma una baadhi ya maelezo sawa lakini yakiwa katika muundo rahisi. Pia unajumuisha maelezo ya ziada ambayo yatakusaidia.

KUMBUKA: Ukiona maneno au istilahi katika Mwongozo huu wa Maelekezo ya iPad ambayo hufahamu, tafadhali angalia ukurasa wa mwisho wenye orodha ya *Fasili ya Maneno ya iPad*.

Vitufe/Vilango:



Jinsi ya Kuweka Chaji iPad Yako:



Hii hapa video ya dakika 35 inayokupa muhtasari wa baadhi ya maelezo msingi kuhusu

iPad kwenye YouTube: <https://bit.ly/iPad-Basics>

Jinsi ya kuweka mipangilio ya iPad yako

1. **Washa:** Bonyeza na ushikilie kitufe cha kuwasha cha iPad hadi uone nembo ya Apple.
2. **Kisha:** Utaona neno "Hello" kwa lugha mbalimbali. Fuata hatua zilizo kwenye skrini ili uanze. (Ikiwa huna uwezo wa kuona au huoni vizuri, unaweza [kuwasha VoiceOver](#) au [Zoom](#) kwenye skrini ya Hello.) Chagua lugha yako ukombwa kufanya hivyo. Kisha bofya jina la nchi yako (Marekani). Chaguo hili linaathiri jinsi maelezo yanavyoonekana, ikiwa ni pamoja na tarehe, saa anwani, na maelezo mengineyo. Kisha, bofya kitufe cha usaidizi kwa watu wenye ulemavu [uweke Chaguo Usaidizi kwa Watu wenye Ulemavu](#) zinazoweza kukusaidia kuweka mipangilio na kutumia iPad yako mpya.




Bofya "[Weka Mipangilio Mwenyewe](#)" kwenye sehemu ya chini ya skrini ili uendelee.

3. **Wezesha:** Unahitaji kuunganisha kwenye mtandao wa Wi-Fi, mtandao wa simu, au iTunes ili uwezeshe na kuendelea kuweka mipangilio ya kifaa chako. Bofya mtandao wa Wi-Fi ambao unataka kutumia au uteue chaguo tofauti.



4. **Weka Kitambulisho cha Kugusa:** Ukiwa na kipengele hiki, unaweza kutumia alama yako ya kidole kufungua kifaa chako na kufanya ununuzi. Bofya Endelea na ufuate maagizo, au ubofye "Weka Mipangilio Baadaye katika Mipangilio."
5. **Unda Nenosiri:** Weka nenosiri lenye nambari sita ili uweze kulinda data yako. Unahitaji nenosiri ili utumie huduma kama vile Kitambulisho cha Kugusa na [Apple Pay](#). Ikiwa ungependa kuweka nenosiri la nambari nne, nenosiri maalum au hungienda nenosiri, bofya "Chaguo za Nenosiri."



6. **Ingia ukitumia Kitambulisho cha Apple:** Weka Kitambulisho chako cha Apple na nenosiri, au bofya "Umesahau nenosiri au huna Kitambulisho cha Apple?" Kutoka hapo, unaweza kurejesha nenosiri au kitambulisho chako cha Apple, kuunda Kitambulisho cha Apple au ukiweke baadaye. Ikiwa unatumia Vitambulisho vingi vya Apple, bofya "Ungependa kutumia Vitambulisho tofauti vya Apple kwa iCloud na iTunes?" Unapoingia kwa kutumia Kitambulisho cha Apple, unaweza kuombwa kuweka msimbo wa kuthibitisha kutoka kwenye kifaa ulichotumia awali.



7. **Washa masasisho otomatiki na uweke vipengele vingine:** Kwenye skrini zinafuata, unaweza kuamua ikiwa ungependa [kuwatumia maelezo](#) wasanidi wa programu na kuruhusu iOS isakinishe masasisho kiotomatiki.



8. **Weka mipangilio ya Siri na huduma nyinginezo:** Utaombwa uweke mipangilio au uwashe huduma na vipengele, kama Siri. Utaombwa utamke maneno machache ili Siri iweze kujua sauti yako. Ikiwa umeingia ukitumia Kitambulisho cha Apple ungependa kuweka [Apple Pay](#) na [iCloud Keychain](#) isiyoyazima, fuata hatua zilizo kwenye iPad.



9. **Weka mipangilio ya Muda wa Kutumia Kifaa na chaguo nyinginezo za kuonyesha:** [Muda wa Kutumia Kifaa](#) hukupa maelezo ya kina kuhusu muda ambao wewe na/au watoto wako hutumia kwenye vifaa. Kipengele hiki pia hukuwezesha kuweka kikomo cha muda wa matumizi ya programu ya kila siku. Baada ya kuweka Muda wa Kutumia Kifaa, unaweza kutumia kipengele cha Upanuzi wa Skrini kubadilisha ukubwa wa aikoni na maandishi yaliyo kwenye Skrini ya Kwanza.



10. **Kamilisha:** Bofya "Anza Kutumia" ili uanze kutumia iPad yako. Hifadhi nakala salama ya data yako kwa [kuhifadhi nakala rudufu](#), na upate maelezo zaidi kuhusu vipengele katika mwongozo wa watumiaji uliokuja na kisanduku cha iPad yako.
11. **Chaji iPad:** Aikoni ya betri ikionyesha kuwa chaji imepungua, unganisha chaja yako. Unajua iPad inachaji wakati aikoni ya betri inaonyesha ishara ya 'radi' ndani yake.



12. **Zima iPad:** Bonyeza na ushikilie kitufe cha **Zima/Washa/Lalisha** kilicho kona ya kuu kulia mwa iPad yako. Endelea kushikilia kitufe hiki hadi kitelezashi kitokee kwenye skrini. Sogeza kitelezeshaji cha **Telezeshu uzime** hadi kulia kabisa.

Kumbuka, maelezo haya na mengineyo yanapatikana kwenye ukurasa wetu wa tovuti wa Digital Inclusion


cv-atlab.org/Digital-Inclusion



Mipangilio ya iPad

Programu ya Mipangilio iko kwenye skrini ya Mwanzo. Ina menu ambayo hufanya mambo mengi:


- Badilisha jinsi tableti yako inavyofanya kazi
- Dhibiti Kitambulisho chako cha Apple na usajili wa App Store
- Zuia maudhui fulani
- Fuatilia na udhibiti jinsi wewe na/au familia yako mnavyotumia kifaa
- Weka mipangilio ya arifa, faragha na nenosiri
- Washa/zima Wi-Fi
- Weka mandhari-nyuma yako
- Badilisha mwangaza wa skrini
- na mambo mengine ZAID!!





Mipangilio ya Usaidizi kwa Watu wenye Ulemavu

iPad ina vipengele vingi vya usaidizi kwa watu wenye ulemavu wa macho, mwili na viungo, masikio na wenye mahitaji na mapendeleo ya kujifunza. Nenda kwenye Mipangilio, kisha utafute aikoni ya Usaidizi kwa Watu wenye Ulemavu:



Kisha chagua kipengele chochote hati ya vifuatavyo. Miongozo na video/viungo maalum kwa kila mojawapo ya vipengele hivi vinapatikana mtandaoni kwenye ukurasa wetu wa wavuti wa Digital Inclusion: www.cv-atlab.org/digital-inclusion


Kuona	Mwili na Viungo	Kusikia
Matamshi	Kugusa	Vifaa vya Kusikia
Kupanua	Kitambulisho cha Uso na Umakinifu	Utambuzi wa Sauti
Kikuzaji	Udhibiti wa Swichi	RTT/TYY
Skrini na Ukubwa wa Maandishi	Udhibiti wa Sauti	Sauti na Picha
Mwendo	Kitufe cha Skrini ya Kwanza au Juu	Manukuu
Maudhui Yaliyotamkwa	Rimoti ya Apple TV	Jumla
Maelezo ya Sauti	Udhibit wa Kielekezaji	Mwongozo wa Ufikiaji
	Kibodi	Siri
	Kalamu ya Apple	Njia ya Mkato ya Usaidizi kwa Watu wenye Ulemavu



Kuweka Mipangilio ya Barua Pepep

Ikiwa unatumia mtoa huduma wa barua pepe kama vile iCloud, Google au Outlook, mipangilio ya Barua Pepe inaweza kuweka akaunti yako ya barua pepe kiotomatiki kwa kutumia nenosiri na anwani yako ya barua pepe:

1. Nenda kwenye Mipangilio  > sogeza chini hadi kwenye **Barua Pepe** > kisha bofya **Akaunti**.
2. Bofya **Weka Akaunti**, kisha chagua mtoa huduma wako wa barua pepe. (Usipo mtoa huduma wako wa barua pepe, bofya **Nyingineili** uweke akaunti yako mwenyewe.)
3. Weka anwani yako ya barua pepe na nenosiri lake.
4. Bofya **Endelea** na usubiri Mail ithibitishe akaunti yako.
5. Chagua maelezo kutoka kwenye akaunti yako ya barua pepe, kama vile Anwani au Kalenda.
6. Bofya **Hifadhi**.





Kuweka Mipangilio ya FaceTime

Katika programu ya FaceTime, unaweza kuwapigia marafiki na familia simu za video au sauti. Unaweza kutumia kamera ya mbele kuzungumza nao ana kwa ana. Badilisha utumie kamera ya nyuma ili uonyeshane mazingira unayoona.

1. Nenda kwenye Mipangilio  > FaceTime, kisha washa FaceTime.
2. Ikiwa unataka kupiga Picha za Moja kwa Moja unapopiga simu za FaceTime, washa Picha za Moja kwa Moja za FaceTime.
3. Weka namba yako ya simu, Kitambulisho cha Apple, au anwani ya barua pepe ya kutumia kwenye FaceTime.





Usalama Mtandaoni/Kwenye Intaneti

Kuna vivinjari kadhaa vya mtandao ambavyo unaweza kutumia kwenye iPad. iPad huuzwa ikiwa na kivinjari cha Safari (aikoni ya dira ya bluu iliyo hapa juu.) Licha ya kivinjari unachopenda, hivi hapa vidokezo 10 kuhusu usalama mtandaoni:

1. Ikiwa wewe ni mgeni kwenye intaneti, omba usaidizi wa mtu unayemwamini.
2. Futa ofa za barua pepe ambazo zinaonekana 'kuahidi makuu yasiyo ya kweli' (utapeli wa kuiba maelezo.)
3. Usishiriki maelezo yako ya binafsi mtandaoni.
4. Soma na uelewe mipangilio ya faragha na sera za faragha za programu.
5. Usiwahi kushiriki manenosiri yako (yaweke faragha/yashiriki tu na watu unaowaamini).
6. Fikiria sana kabla ya kusema chochote mtandaoni. Unachosema kinaweza kushirikiwa na watu wengi.
7. Mtu akisema kitu mtandaoni kinachokukasirisha, mwambie mtu unayemwamini.
8. Usipakue au kubofya viungo isipokuwa unajua vinaaminika.
9. Unapotumia Wi-Fi ya umma (kama ya mkahawani) usiweke maelezo ya kibinafsi au ya kifedha kwenye tovuti.
10. Hakikisha unatumia toleo jipya la programu-tumizi.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu usalama mtandaoni, tembelea:

www.usa.gov/online-safety

Kumbuka, maelezo haya na mengineyo yanapatikana kwenye ukurasa wetu wa tovuti wa Digital Inclusion

cv-atlab.org/Digital-Inclusion

Fasili ya Maneno ya iPad

Programu: Ufupisho wa “programu ya simu.” Kila aikoni iliyo kwenye skrini ya iPad yako inawakilisha "programu" inayofanya kazi maalum, kama vile barua pepe, kivinjari cha mtandao, nk.

Kitambulisho cha Apple: Jina la mtumiaji na nenosiri maalum ukitumia anwani yako ya barua pepe na nenosiri unayotaka. Inahitajika kuweka mipangilio ya iPad yako na kupakua programu, ikiwa ni pamoja na programu zilizolipishwa.

Bluetooth: Njia pasiwaya ya kuunganisha zana kwenye iPad, kama vile kibodi, spika, kalamu ya Apple, vipokea sauti au vifaa vingine. Vifaa vya Bluetooth vinaweza kuunganishwa na iPad yako katika menyu ya Mipangilio, kisha kwenye kichupo cha "Bluetooth".

Pini ya Kipokea Sauti: Tundu dogo la duara kwenye ukingo wa juu kushoto wa iPad ambapo kebo ya kipokea sauti inaunganisha kwenye iPad.

Kitufe cha Skrini ya Kwanza: Kitufe cha duara, cha ukubwa wa sumuni kwenye sehemu ya chini kati ya uso wa iPad ambacho hutumiwa kubofya kwenye skrini unayotumia ili urudi "mwanzo" - ukurasa ambapo programu zako zimepangwa. Inaweza pia kubofwa mara moja ili "kuamsha" iPad wakati skrini imezimwa au 'imelala'. Kitufe cha ukurasa wa kwanza pia ni mahali ambapo utaweka kidole chako wakati unatumia Kitambulisho cha Kugusa ili kufungua iPad yako.

Mtandao/Kivinjari cha Wavuti: Programu au inayokuwezesha kutafuta maudhui na kutumia intaneti/mtandao. Vivinjari vinavyotumika mara nyingi Safari, Google Chrome na Firefox.

iOS: Mfumo wa Uendeshaji wa Apple wa iPads na iPhones unaitwa iOS. Mfumo wa uendeshaji ni jina la kifurushi cha programu-tumizi kinachoendesha kompyuta au kifaa chako, na mara nyingi huwa na namba mwishoni ambazo hukufahamisha toleo la mfumo unalotumia. Kwa mfano, hivi sasa toleo jipya zaidi la iOS ni iOS 14.2. Unapaswa kusasisha mfumo wako wa uendeshaji mara kwa mara kwenye menyu ya Mipangilio chini ya sehemu ya "Jumla."

Lango Nishati: Tundu dogo la umbo bapa kwenye ukingo wa chini kati wa iPad ambapo kebo ya kuchaji inaunganisha kwenye iPad. Vipokea sauti vipya vya waya vya Apple vinaweza pia kuunganishwa hapa.

Kiunganishi cha Nishati: Kebo inayotumika kuchaji iPad au kuiunganisha na vifaa vingine kama kompyuta. Upande wake mmoja ni mdogo na bapa na huingia katika lango la nishati la iPad. Upande mwingine ni kiunganishi kikubwa cha mstatili cha USB ambacho huingia kwenye chaja au kwenye lango la USB kwenye kompyuta au kifaa kingine.

Kuiba maelezo: Aina ya barua pepe au utapeli wa mtandaoni. Utapeli wa kuiba maelezo kawaida huwa kiungo au kiambatisho kilicho kwenye barua pepe au ukurasa wa wavuti ambao unaweza kuiba maelezo yako ya kibinafsi ukikibonyeza. Ukipokea barua pepe kutoka kwa mtu usiyemjua, au kutoka kwa orodha ya barua pepe ambazo hukumbuki ukijisajili kupokea, kuwa mwangalifu Usibofye viungo au viambatisho vyovyote vinavyoonekana kutiliwa shaka.

Kitufe cha Kuwasha: Kitufe bapa cha mstatili kwenye ukingo wa juu kulia wa iPad yako. Kitufe hiki kinaweza kutumiwa kuwasha/kuzima iPad yako, kwa kukishikilia hadi skrini ionyeshe maelezo ya kuzima/kwenye skrini. Ukibofya mara moja utaamsha au kulalisha/kuzima skrini ya iPad yako.

Siri:Programu iliyo katika iPad yako ambapo unaweza kutumia sauti yako kuuliza maswali na kutoa maelekezo. Siri inaweza kupokea maswali yanayotamkwa na kufanya mambo yanayojumuisha kufungua programu, kupiga simu, kuendeleza au kusoma ujumbe na barua pepe, au kujibu maswali kupitia intaneti.

Kitambulisho cha Kugusa: Mipangilio ya usalama ya Apple inayokuwezesha kufungua iPad yako ukitumia alama ya kidole chako. Angalia maagizo ya kuweka mipangilio hapa juu. Baada ya kuweka mipangilio ya iPad yako, unaweza kuweka alama ya vidole zaidi ikiwa ungependa.

Wi-Fi: (ufupisho wa 'wireless fidelity') Huduma ya kununuliwa ambayo inawezesha vifaa kama iPads, simu mahiri, kompyuta na printa kufikia intaneti na kuwasiliana na vifaa vingine vikunganishwa kwenye huduma/mtandao mmoja wa Wi-Fi. Unaweza kuweka Wi-Fi nyumbani kwako au unaweza kuipata kwenye mkahawa au duka kubwa (kama duka la vyakula.)

Tunatambua na Kushukuru:

Usaidizi kwa Wateja wa Apple mtandaoni kwenye support.apple.com. Kiasi kikubwa cha maudhui yaliyo kwenye Mwongozo huu wa Maelekezo ya iPad yanatokana na kazi ya Usaidizi kwa Wateja wa Apple.

Jiji la Portland na mradi wa CARES Act Project walitoa usaidia kupitia [Sheria ya Fedha za Usaidizi wa Kifedha wa Eneo wa CARES](#), ulioidhinishwa na Halmashauri ya Jiji la Portland kukabiliana na athari za COVID-19 kwa jamii zilizoathiriwa zaidi. Hazina hii ilifadhili iPads, teknolojia ya kutoa usaidizi, usambazaji na mafunzo kwa mamia ya Wanaportland. Tunatoa shukrani za kipekee kwa Kundi Kazi la Digital Divide kwa juhudi zao za kukabiliana na COVID-19 na juhudi nyingine zote.